TANGAZO LA SERIKALI NA. 590 la tarehe 30/9/2022

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA)

(SURA YA 287)

# SHERIA NDOGO

*(Zimetungwa chini ya kifungu cha 153)*

SHERIA NDOGO (HIFADHI YA MAZINGIRA) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA NSIMBO ZA MWAKA 2022

Jina

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Hifadhi ya Mazingira) za Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo za mwaka 2022 .

Eneo la matumizi

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote lililo chini ya mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa itakapoelezwa vinginevyo:

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo na ni pamoja na Afisa yeyote wa umma atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"Afisa muidhiniwa" maana yake ni Afisa yeyote wa Halmashauri atakayeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi;

"Eneo la Hifadhi" ni maeneo ya milima, maeneo ya vyanzo vya maji, hifadhi ya misitu, miteremko na maeneo mengine ambayo yatatangazwa na Halmashauri kuwa ni maeneo ya hifadhi;

"Hifadhi ya Mazingira" maana yake ni utunzaji endelevu wa ardhi, mimea, hewa, viumbe hai na visivyo hai na vyanzo vya maji vinavyozingatia

masharti na maelekezo yatakayotolewa na Afisa muidhiniwa chini ya Sheria Ndogo hizi au Sheria nyingine yeyote;

"Kiwanda" maana yake ni jengo au kundi la majengo au eneo ambapo vitu vinatengenezwa;

"Kuvuna misitu" maana yake ni pamoja na kufyeka, kukata au kung'oa miti na visiki;

"Maeneo ya malisho" maana yake ni pamoja na sehemu zote ambazo zimetengwa na Halmashauri kwa ajili ya kuchungia wanyama wa kufugwa;

Sura 191 "Maji" Maana yake ni kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira;

Sura 191 "Maji taka" Maana yake ni kama ilivyo katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira;

Sheria Na 14 ya 2002 "Mazao ya misitu" maana yake kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Misitu;

Sura 191 "Mazingira" Maana yake ni kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira;

"Mfugaji" maana yake ni mtu yeyote anayejishughulisha na ufugaji mifugo katika eneo la Halmashauri;

"Mifugo" maana yake ni mnyama yeyote anayefugwa na binadamu,

Sura 191 "Misitu" maana yake ni kama ilivyotafsiriwa na Sheria ya Misitu;

Sura 191 "Taka" Maana yake ni kama ilivyo katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira;

Sura 191 "Taka ngumu" Maana yake ni kama ilivyo katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira;

Sura 191 "Taka za viwandani'' Maana yake ni kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira;

Sura 191 "Uchafu hatari" Maana yake ni kama ilivyotafsiriwa katika sheria ya usimamizi wa mazingira;

Sura 191 "Uchafuzi wa Mazingira" Maana yake ni kama

ilivyo katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira;

## SEHEMU YA PILI
## MASHARTI YA UFUGAJI

Wajibu wa mfugaji

4. Kila mfugaji chini ya Sheria Ndogo hizi:-

(a) atatakiwa kufuga mifugo kama itakavyoainishwa katika kibali chake kitakachomruhusu kufuga kwa kuzingatia ukubwa wa eneo na kuridhika kwamba ufugaji huo hautakuwa kero kwa majirani.

(b) atatakiwa kufuga ndani ya eneo lake (zero grazing) bila ya kuleta usumbufu kwa jirani zake na jamii kwa ujumla na kuhakikisha sehemu ya kufugia wanyama hao inakuwa safi wakati wote na ana chombo cha kuhifadhi samadi inayotokana na mifugo hiyo.

(c) atatakiwa kupitisha mifugo yake katika njia zilizopangwa na kuidhinishwa na Halmashauri.

(d) atatakiwa kuwa na kadi ya mifugo itakayoonyesha idadi na aina ya mifugo aliyonayo;

(e) atatakiwa kupeleka mifugo katika majosho kama atakavyoagizwa na Halmashauri;

(f) atatakiwa kupeleka mifugo yake katika vituo vya chanjo kama itakavyoamuriwa na Halmashauri na atalipia chanjo hiyo kama atatakiwa kufanya hivyo;

Masharti ya ufugaji

5. Ni marufuku kwa mfugaji yeyote:-

(a) Kuingia kwenye msitu wa hifadhi na vyanzo vya maji na kufanya shughuli za ufugaji ambazo ni pamoja na kuchunga, kulisha na kunywesha maji mifugo au kufanya shughuli hizo katika maeneo ya mipango miji na maeneo yote ambayo hayakutengwa kwa ajili hiyo;

(b) kusafirisha mifugo kwa kuiswaga barabarani;

(c) kusafirisha au kuhamisha mifugo kutoka eneo moja hadi jingine bila kibali kutoka kwa Halmashauri;

(d) kuuza au kununua mifugo katika maeneo ambayo siyo mnada, masoko au magulio ya mifugo yaliyoidhinishwa na Halmashauri; au

(e) kupitisha mifugo katika maeneo ambayo hayakuidhinishwa na Halmashauri kupitisha mifugo;

Kudhibiti mifugo inayozurura ovyo

6. (1) Halmashauri itakamata mifugo au mfugo wowote utakaoonekana unazurura hovyo katika eneo la Halmashauri ambapo hapajaruhusiwa kuchungia mifugo.

(2) Mfugo wowote utakaokamatwa utalipiwa faini kama ilivyooneshwa kwenye jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hizi na baada ya kulipia gharama hizo mfugaji atarudishiwa mifugo yake.

(2) Endapo mwenye mifugo au mfugo hatatokea ndani ya siku saba (7) tangu kukamatwa kwa mifugo hiyo, Mkurugenzi wa Halmashauri atakuwa na haki ya kuuza kwa mnada mfugo au mifugo hiyo baada ya kupata idhini ya Mahakama.

(3) Baada ya mauzo, Mkurugenzi atakata fedha za faini, gharama za mnada na gharama za ulinzi na fedha zitakazobaki atapewa mwenye mifugo na kama hataonekana ndani ya siku kumi na nne (14) fedha hizo zitaingizwa katika vyanzo vya mapato ya Halmashauri.

(4) Endapo mwenye mifugo hiyo atakuwa na sababu za msingi za kutofika kwake katika muda wa siku kumi na nne (14) Halmashauri itarudisha fedha zake

Ukaguzi wa mifugo

7. (1) Afisa Mwidhiniwa anaweza kuingia katika nyumba au jengo lolote wakati wowote kwa madhumuni ya kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi.

(2) Mtu yeyote atakayemzuia afisa Muidhiniwa kutekeleza wajibu wake chini ya Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa.

Wajibu wa Halmashauri

8. (1) Itakuwa ni wajibu wa Halmashauri kutenga maeneo maalum kwa ajili ya shughuli za malisho kwa kuzingatia idadi ya mifugo ndani ya eneo la Halmashauri.

(2) Halmashauri itatenga njia maalum za kupitisha mifugo kwenda na kurudi malishoni au minadani.

(3) Halmashauri itafanya sensa ya mifugo na kutoa kadi za mifugo na elimu ya ufugaji bora kwa jamii.

Taratibu za ufugaji

9. (1) Wafugaji wote watatakiwa kuzingatia masharti ya kufuga kama yalivyo katika Sheria Ndogo hizi au Sheria yoyote iliyotungwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

(2) Kila mfugaji atatakiwa kupeleka mfugo au mifugo yake machinjioni au mahali huduma hiyo inapopatikana na itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote kuchinjia nyama mahali pengine popote ambapo sio machinjio. Mtu yoyote atalazimika kulipia gharama za machinjio pale anapochinja mfugo au mifugo yake katika machinjio ambapo kwa kila ng'ombe itakuwa ni Tshs.1,500 na mbuzi Tshs. 1,000

(3) Ni marufuku kwa mtu yeyote kununua, kuuza au kufanya biashara ya kubadilishana aina yoyote ya mifugo katika eneo lolote la Halmashauri isipokuwa kwenye minada au magulio yaliyotengwa kwa shughuli hiyo.

(4) Mtu yeyote atakayekuwa anasafirisha mnyama au wanyama kwenda mnadani, nje au ndani ya eneo la Halmashauri lazima awe na kibali kutoka kwa Mtendaji wa Kijiji husika kuthibitisha uhalali na

umiliki wa mnyama au wanyama husika.

## SEHEMU YA TATU
## KILIMO NA HIFADHI YA ARDHI

Taratibu za kilimo

10. (1) Mtu atakayetaka kuendesha shughuli za kilimo katika Halmashauri atatakiwa kuzingatia taratibu za kilimo kama zitakavyotolewa na Halmashauri.

(2) Afisa Mwidhiniwa anaweza kuingia katika shamba lolote kwa madhumuni ya kufanya ukaguzi na kuhakikisha utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi.

Masharti kwa mkulima

11. (1) Ni marufuku kwa mtu yeyote kulima katika miteremko, karibu na vyanzo vya maji, kandokando ya mito, mabwawa na maziwa au kufanya jambo lolote litakaloharibu hifadhi ya mazingira bila kuzingatia ushauri wa afisa kilimo.

(2) Ni marufuku kwa mtu yeyote kutumia kinyume ardhi iliyotengwa kwa matumizi ya kilimo kama ilivyopangwa na kuidhinishwa na Halmashauri.

(3) Ni marufuku kwa mtu yeyote kusafisha shamba kwa ajili ya kilimo kwa njia ya kuchoma moto isipokuwa kwa kibali maalum kutoka Halmashauri.

(4) Kibali kitakachotolewa chini ya Sheria Ndogo hizi kitakuwa cha maandishi na kitaonyesha jina la mwenye kibali, tarehe na eneo analotaka kuchoma moto.

(5) Muda unaotakiwa kuchoma moto chini ya Sheria Ndogo hizi ni kuanzia saa 12:00 asubuhi hadi saa 4:00 asubuhi.

(6) Ni wajibu wa Halmashauri kusimamia shughuli za kilimo na kuhakikisha kuwa wanazuia kilimo cha kuhamahama na kuhimiza kilimo cha mzunguko.

Uhifadhi wa uoto wa asili

12. Ni wajibu wa wakazi wa eneo ambalo uoto wa asili au mazingira ya eneo husika yameharibiwa, kuhakikisha kuwa wanalirudisha katika hali yake

ya kawaida kwa kupanda miti au kutoendelea kuharibu mazingira na kuwezesha uoto urudi katika hali yake.

Uchimbaji mchanga na kokoto

13. Ni marufuku kwa mtu yeyote kuchimba mchanga katika maeneo yasiyoruhusiwa na Halmashauri kama vile katika maeneo ya makazi ya watu, maeneo yaliyohifadhiwa kando kando ya barabara, mito au ndani ya mto, bwawa au ziwa katikati ya barabara.

Ujenzi na ufyatuaji wa tofali

14. (1) Ni marufuku kwa mtu yeyote kufyatua na au kujenga nyumba au jengo lolote katika eneo la hifadhi.

(2) Kila Kijiji kitatenga maeneo maalumu kwa ajili ya ufyatuaji wa tofali ikiwa ni pamoja na benki ya tofali kwa ajili ya ujenzi wa majengo ya umma au maendeleo.

## SEHEMU YA NNE
## HIFADHI YA VYANZO VYA MAJI

Wajibu wa kulinda vyanzo vya maji

15. (1) Halmashauri itawajibika kuanzisha, kusimamia na kulinda vyanzo vya maji.

(2) Maeneo yaliyotajwa katika Jedwali la Pili katika Sheria Ndogo hizi yamehifadhiwa

(3) Halmashauri itachukua hatua kali za kisheria dhidi ya mtu yeyote atakayeharibu chanzo cha maji au kushindwa kushiriki katika shughuli za kuhifadhi ya vyanzo vya maji bila sababu ya msingi.

Kulinda eneo la hifadhi

16. (1) Ni marufuku wa mtu yeyote kulima, kukata miti, kufuga mifugo katika umbali wa mita 60 kutoka kwenye vyanzo vya maji au kufanya jambo lolote linaloharibu kwa namna yoyote chanzo cha maji na hifadhi ya mazingira.

(2) Itakuwa ni wajibu wa Halmashauri kupanda miti isiyonyonya maji katika vyanzo vya maji kwa kuzingatia maelekezo ya afisa misitu.

(3) Ni marufuku kwa mtu yeyote kumiliki eneo la chanzo cha maji isipokuwa kwa ruhusa ya Halmashauri.

Uchafuzi wa vyanzo vya maji

17. (1) Ni marufuku mtu yeyote, kiwanda, taasisi, shirika kuelekeza mabomba ya maji machafu kwenye mito, mabwawa, visima, mifereji, chemichemi au sehemu yoyote ambayo ni chanzo cha maji kwa ajili ya matumizi ya binadamu na wanyama au viumbe vingine vilivyo hai.

(2) Ni marufuku mtu yeyote kuweka kitu chochote chenye sumu ndani ya maji ambayo yanatumiwa na binadamu au kiumbe chochote hai.

## SEHEMU YA TANO
## HIFADHI YA MISITU

Kuchoma au kusababisha moto

18. (1) Ni marufuku kwa mtu yeyote kuchoma misitu kwa namna yoyote ile katika misitu iliyoko eneo la Halmashauri.

(2) Iwapo moto utatokea katika eneo la Halmashauri, kiongozi wa eneo husika atawajibika kutoa ishara ya hatari kwa kutumia njia iliyozoeleka kuamuru wakazi wa eneo hilo kwenda kuzima moto huo unapoonekana kuwa na madhara kwa maisha, mali za watu na uharibifu wa mazingira katika eneo hilo.

(3) Kila mkazi wa eneo hilo atawajibika kushiriki katika zoezi la kuzima moto huo endapo atatakiwa kufanya hivyo, kama atashindwa kushiriki katika kuzima moto bila sababu ya msingi atakuwa ametenda kosa.

Kibali cha kuchoma moto

19. Mtu yeyote aliyepata kibali cha kuchoma moto atalazimika kutoa taarifa ya siku saba (7) kabla ya kuchoma moto kwa majirani walioko katika eneo analotaka kuchoma na ataweka njia za kuzuia moto.

Ukataji miti na kuni

20. (1) Ni marufuku kwa mtu yeyote kukata miti au kuni katika maeneo ya misitu iliyohifadhiwa kwa ajili ya matumizi ya aina yoyote bila kupata kibali kutoka Halmashauri.

(2) Halmashauri itatakiwa kuhakiki kama miti inayovunwa imekomaa na inafaa kwa ajili ya matumizi.

(3) Ni marufuku kwa mtu yeyote kuvuna miti katika msitu ambao umehifadhiwa kwa ajili ya viumbe maalum ambao ni rasilimali kwa Taifa.

(4) Watu wanaovuna miti kwa ajili ya kuchoma mkaa watatakiwa kuwa na eneo maalum lililoidhinishwa na Halmashauri kwa ajili ya kuchoma mkaa kwa vibali maalumu.

Wajibu wa kupanda miti

21. Kila mkazi wa Halmashauri atawajibika:-
(a) kupanda na kutunza miti katika eneo lake.
(b) kupanda na kutunza miti katika shamba au mashamba anayomiliki.

Wajibu wa Kijij

22. Kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi kila kijiji:-
(a) chenye eneo la kutosha kitawajibika kutenga eneo la hifadhi ya misitu ya asili kwa ajili ya matumizi ya baadaye;
(b) kitalazimika kutunza miti yote inayopandwa katika eneo la kijiji;
(c) kitahakikisha kuwa kila kaya inapanda miti isiyopungua kumi ikiwemo ya matunda kwenye eneo la nyumba yake;
(d) mtu yeyote anayetaka kukata miti au mti

wa matumizi yakuchonga vifaa, kujenga nyumba, kutengeneza zizi na shughuli nyinginezo, inabidi apate kibali cha maandishi kutoka kwa mwenyekiti wa kijiji, mtendaji wa kijiji na kibali cha afisa maliasili wa wilaya au wasaidizi wake kwa miti iliyopanda na kuhifadhiwa na Halmashauri;

(e) kinapaswa kutenga na kupanda shamba la miti ekari 2 kila mwaka na kulitunza;

(f) kila shule au taasisi nyingineyo katika Halmashauri itapaswa kupanda miti ya kukinga upepo kuzunguka eneo lake;

(g) Kijiji kitapaswa kutunza na kuhifadhi miti na nyasi kwenye milima, makorongo na vyanzo vya maji ili kuzuia mmomonyoko wa udongo;

(h) Kijiji kitahakikisha kuwa kila anayeandaa shamba kwa ajili ya kilimo hatumii moto na anapanda miti kwenye mipaka ya shamba lake kama kinga upepo;

(i) Kila mtu mwenye nyumba kwenye eneo la kati la kijiji atawajibika kupanda miti kando ya barabara inayopita mbele ya nyumba yake na kuitunza;

(j) Kila mwenyekiti wa kijiji, mtendaji wa kijiji, mkuu wa taasisi yoyote atahakikisha kuwa kuna msitu wa hifadhi wa miti ya kupandwa au ya asili iliyotengwa kwa madhumuni ya kuhifadhi ardhi, mazingira na matumizi ya baadaye.

## SEHEMU YA SITA
## HIFADHI (MAKABURI)

Makaburi na mazishi

23. (1) Ni wajibu wa Halmshauri kutenga maeneo ya makaburi na kuhakikisha maeneo hayo yanakuwa katika hali ya usafi na usalama wakati wote.

(2) Ni marufuku kwa mtu yoyote kuzika mwili

wa binadamu katika eneo ambalo halikutengwa na Halmashauri kwa ajili ya shughuli hiyo.

(3) Iwapo mtu yeyote atataka kuzika eneo tofauti na lililotengwa atapaswa kuomba kibali kutoka Halmashauri.

## SEHEMU YA SABA
## TAKA NGUMU NA LAINI

Taka ngumu na laini

24. (1) Ni wajibu wa Halmashauri kutenga eneo kwa ajili ya kutupa taka ngumu na laini na kusimamia kwa karibu usafi katika eneo lake kwa kutumia rasilimali zake au kupitia vikundi vya usafi vilivyosajiliwa kwa ajili ya shughuli za usafi.

(2) Mtu yeyote atakayetupa ovyo taka ngumu au laini, au kujisaidia/kuoga katika kingo za mabwawa, mito au kwenye vyanzo vya maji vilivyoko katika Halmashauri atakuwa ametenda kosa chini ya Sheria Ndogo hizi.

Kibali cha uendeshaji wa viwanda

25. Ni marufuku kuendesha shughuli za karakana, mashine ya kusaga, kuranda mbao, kukamua maji ya matunda, kuchomelea vyuma au kuendesha shughuli yoyote inayozalisha uchafu ambao unaleta athari kwa binadamu na viumbe wengine katika maeneo ya makazi ya watu bila kibali na kuzingatia taratibu za ujenzi.

## SEHEMU YA NANE
## MAKOSA NA ADHABU

Makos ana adhabu

26. Mtu yeyote atakayekwenda kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na endapo atapatikana na hatia atatozwa faini isiyozidi shilingi laki tatu(300,000/=) au kutumikia kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili au kutumikia adhabu zote kwa pamoja.

Kufifilisha 27. Mkurugenzi anaweza kumtoza mtu yeyote faini ya shilingi elfu hamsini (50,000/=) iwapo mkosaji atakiri kosa kwa maandishi na kukubali kutekeleza wajibu wake pamoja na kulipa faini anayodaiwa kwa kujaza fomu ya kukiri kosa iliyoainishwa kwenye Jedwali la Tatu la Sheria Ndogo hizi.

JEDWALI LA KWANZA

(Limetungwa chini ya kifungu cha 6 (2)

Faini ya mifugo kuzurura hovyo

| | |
|---|---|
| Faini ya Mifugo iliyokamatwa ikizurura ovyo | 50,000 kwa Ng'ombe<br><br>30,000 kwa Mbuzi na Kondoa |

JEDWALI LA PILI

Maeneo yaliyohifadhiwa ndani ya Halmashauri

*(Chini ya Kifungu cha 15(2))*

| NA | ENEO LILILO HIFADHIWA | KIJIJI/MTAA ENEO LILIPO/LINAPOPITIA | KATA |
|---|---|---|---|
| 1 | Mto Rulenke | Litapunga (Kaburonge B) hadi Kanoge | Litapunga,Kanoge na Ugalla |
| 2 | Mto Ugalla | Ugalla (Katambike) | |
| 3 | Mto Shura | Uruwira (Ikondamoyo) hadi Usense | Uruwira |
| 4 | Mto Msaginya | Katumba (Sokoine), Nsimbo hadi Sitalike | Katumba, Nsimbo na Sitalike |
| 5 | Mto Shelesi | Mtapenda (Mtapenda) | Mtapenda |
| 6 | Mto Mnyamasi | Ugalla (Mnyamasi) hadi Kasisi | Ugalla |
| 7 | Mto Nzaga | Katumba (Nzaga) hadi Uruwira | Katumba na Uruwira |
| 8 | Kiholo | Katumba (Ivungwe) | Katumba |
| 9 | Kalabi | Uruwira (Uruwira) hadi Nsimbo | Uruwira na Nsimbo |
| 10 | Mto Katuma | Sitalike hadi Intenka | Sitalike na Itenka |
| 11 | Kenswa | Katumba (Sokoine) hadi Nsimbo (Msaginya) | Katumba na Nsimbo |
| 12 | Kajeje | Kanoge (Kajeje B) hadi Ndurumo Mtapenda | Kanoge na Mtapenda |
| 13 | Kabuga | Kanoge (Kabuga) | Kanoge |
| 14 | Kosovo | Litapunga (Bulembo) | Litapunga |

*Tangazo La Serikali Na. 590 (Linaendelea)*

| | | | |
|---|---|---|---|
| 15 | Mto Nsanda | Litapunga | Litapunga |
| 16 | Nduwi Station | Katumba (Nduwi Station) | Katumba |
| 17 | Ikolongo | Mtapenda (Ikolongo B) | Mtapenda |
| 18 | Mshiha | Kanoge (Kanoge Laini) | Kanoge |
| 19 | Mto Mtambo | Katumba (Ivungwe) | Katumba |
| 20 | Mto Kaninka | Uruwira (Ikondamoyo) | Uruwira |
| 21 | Mto Utobe | Katumba hadi Uruwira (Uruwira | Uruwira na Katumba |
| 22 | Silasi | Mtapenda (Isinde) | Mtapenda |
| 23 | Milumbani | Mtapenda (Mtapenda) | Mtapenda |
| 24 | Mto Ndurumo | Mtapenda hadi Katumba | Katumba na Mtapenda |
| 25 | Kanyantumbi | Mtapenda (Mtapenda) hadi Nsimbo | Mtapenda na Nsimbo |

## JEDWALI LA TATU

(Limetungwa chini ya Kifungu cha 27)

KUFIFILISHA KOSA

FOMU YA KUFIFILISHA KOSA

Mimi .......................................................................................... wa S. L. P. ..................... ninaefanya shughuli ya .................................. katika eneo la ........................................................................ lililopo ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo. Nakiri kuwa leo tarehe .................................... nilikiuka kifungu cha .................................... cha Sheria Ndogo za (Hifadhi ya Mazingira) za Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo za mwaka 2022. Kwa hiyo, kwa hiari yangu mwenyewe na bila kushawishiwa na mtu yeyote, nakubali kulipa faini iliyoainishwa kwenye Sheria Ndogo hizi iwapo Mkurugenzi atatekeleza madaraka aliyopewa chini ya Fungu la 27 la Sheria Ndogo hizi.

Hivyo basi nakubali kulipa kiasi cha Tshs. ..............................kama faini kwa makosa/kosa .......(idadi) chini ya vifungu tajwa hapo juu nilivyokiuka.

Saini ya Mtenda Kosa: ............................................................

Mbele ya:-

Jina ..........................................................................................

Saini ..........................................................................................

Wadhifa ......................................................................................